

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



*Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
Barabara ya Hospitali,
Jengo la Mkapa
S.L.P. 1923,
DODOMA.*

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CCD. 215/401/01

28 Desemba, 2017

Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa,
TANZANIA BARA

**YAH: KUCHELEWA/KUKATAA KUPITISHA BARUA ZA WATUMISHI
WANAOHAMISHWA KWA KIBALI CHA KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

Tafadhali husikeni na somo tajwa hapo juu.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI imebaini kuwa kuna kuchelewa au kusita kupitisha barua za watumishi waliohamishwa kwa kibali cha Katibu Mkuu - TAMISEMI. Watumishi waliohamishwa wamekuwa wanazungushwa na Wakuu wa Idara za Utumishi za Halmashauri zenu bila kuwepo sababu za msingi. Tafsiri ya haraka ni kuwa bado Ofisi zenu zinaendeleza vitendo vya Rushwa ndiyo sababu watumishi wanasumbuliwa sana!

Mara nyingi watumishi hao wenye barua za uhamisho wamekuwa wanaambiwa tunataka tujiridhishe kama barua zao ni halali na hivyo Halmashauri zinasema zimetuma barua Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhoji uhalali wa barua hizo za uhamisho. Tunajiuliza, barua imesainiwa na Katibu Mkuu na kutangazwa kwenye tovuti ya TAMISEMI huo uthibitisho unatafutwa una lengo gani??

Nataka niwakumbushe kuwa, uhamisho wa Watumishi walioomba wenyewe una sababu za msingi ndiyo maana Ofisi ya Rais - TAMISEMI imekubali. Ofisi

za Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukataa au kuchelewa kwa makusudi kupitisha barua hizo na kuweka hoja nyepesi za kujiridhisha ni dalili za wazi za kuendeleza vitendo vya Rushwa. Tuna taarifa kuwa wale wanaopitishiwa barua zao haraka haraka ni wale tu wanaokubaliana na matakwa ya Maafisa wenu kupewa rushwa! Jambo hilo likome mara moja!!

Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kubaini maofisa wenye tabia hiyo na kuwachukulia hatua kali. Wanaotajwa sana ni Maafisa Elimu (kwa walimu) na Maafisa Utumishi (kwa watumishi wote). Mkurugenzi atakayeshindwa kuwadhibiti watumishi waliochini yake ambao wanajihusisha na vitendo vya RUSHWA atakuwa ameshindwa madaraka ya Ofisi.

Nashukuru kwa ushirikiano wenu.



Eng. Mussa I. Iyombe
KATIBU MKUU

Nakala: Makatibu Tawala wa Mikoa
TANZANIA BARA